

## **Wanaolipa Madeni Yao Ni Wema au Mabwege?**

Watu wazima wengi wataukumbuka wimbo wa Bob Dylan alipoimba mnamo 1963, “Nyakati hubadilika” na kila siku najiuliza, nyakati hubadilika kwa mema? Hili, “mimi kwanza”, “nimepata...” na “nitapata...”, aina ya jamii ya kimwili tuishiyo ndani yake siku hizi imebadilika, au uvunjwaji wa akiba zetu benki, kustaafu, majumbani, familia, maadili, desturi, miiko, n.k.

Twaishi katika siku ambazo, kama unataka kitu na endapo una mkopo kidogo, unaweza kukipata; bila kujali unaweza kulipa au la. ‘Matashi’ yetu huipelekesha tabia yetu ya matumizi hata kufikia hatua ya kwamba wengi leo hawana uelewa wa tofauti baina matashi na haja. Hukumbuki kipindi cha uchumi kwenye elimu ya juu? Somo juu ya matashi na mahitaji? Naam, natambua, mistari ina maluweluwe!

Hivyo, siku hizi Wamarekani mamilioni wameweka rehani, mikopo ya magari, kadi za mikopo juu ya kadi za mikopo. Pamoja na mikopo yote hii, mamilioni ya watu leo wana kila kitu cha kukidhi kidogo matamanio ya mioyo. Siku moja, mamilioni ya watu hawa watatizama madeni yao na kutambua “tunatumia zaidi ya nyenzo tulizo nazo, tumeingia kwenye tatizo, na hatuna tena uwezo wa kuyalipa madeni.” Hivyo, ni lazima maamuzi yachukuliwe, na mazoea lazima yasitishwe. Hat hivyo, ni vigumu kusitisha mazoea kwa sababu ya uchu wa kutaka kuwa na kila usicho nacho. Sasa, unaweza kupata vyote, na deni na maumivu ya moyo ambayo huambatana navyo vilevile.

Hivyo, unaenda kazini, ili kudunduliza kiasi ambacho hakiwezi halipa kiasi unachodaiwa. Sasa, kwa Wamarekani wengi, hivi, nani alaumiwe? Hakuna aliyekulazimisha ununue nyumba kubwa, gari jipya na zuri, na kila kifaa kidogodogo. Hivyo, mtu wa Mungu anafanyaje, anapojikuta yuko katika mvurugiko wa kiuchumi wa kujitakia? Mweke tu mtu wa Mungu: 1) ataitunza familia yake, 1 Timotheo 5:8. 2) Atajifunza kuishi kulingana na mahitaji yake, Wafilipi 4:10ff. 3) Atalipa madeni yake, Warumi 13:8. 4) atakuwa wakili mwaminifu kwa Bwana, Luka 16:10-13. 5) na mtu wa Mungu atashika ahadi au

mapatano aliyofanya na baina yake na taasisi za kifedha, Hesabu 30:2; Zaburi 89:34.

*“nyakati, zinabadilika.”* Kuna wakati ambapo tamshi lako lilikuwa dhamana yako. Na kama ulisema ungelipa, ulilipa. Lakini sasa tunaishi katika zama ambazo asilimia 36 ya Wamarekani huamini kuwa kimaadili na kwa mujibu wa miiko ni halali kuyakimbia madeni binafsi waliyojisababishia kwa sababu waliona maluweluwe kwenye mistari. Wapo Maprofesa na waandishi wanaofundisha *“kama hutaki kulipa ulichoahidi kulipa, basi usilipe, kimbia, na warudishie”* Siku hata imefikia wafilisi wanawashauri wale waliolemewa na madeni ya mikopo, kutolipa madeni yao!

Kwa sababu tu tunaishi katika *“mazingira ya biashara holela,”* Hilo halitupi kibali cha kuishi kidhalimu. Umewahi kusikia kwamba *“makosa mawili hayafanyi kuwa sahihi.”* Na sasa, kwa kuwa watu wengi wameyakimbia madeni yao, wakati wangetekeleza ahadi zao, sasa mabenki hayakopeshi tena. Na kwa nini wakopeshe? Kwa sababu imekuwa dhahiri mno kwao kwamba sisi Wamarekani hatutambui tena *“mema na mabaya.”* Ni kweli, Mkristo anatakiwa kujua ni lipi jambo sahihi la kufanya i. Swali ni, *“unamwamini Mungu kwamba atakutunza?”* Wakati unafanya yakupasayo, kalipa madeni uliyoahidi kulipa, Mathayo 6:25-34.